

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



WIZARA YA AFYA

TAARIFA KWA UMMA KUHUSU TETESI ZA UWEPO WA UGONJWA USIOJULIKANA MKOANI KAGERA

DODOMA, 16 Machi, 2023.

Ndugu Wananchi, Wizara imepokea taarifa za uwepo wa ugonjwa ambao bado haujajulikana mkoani Kagera katika wilaya ya Bukoba Vijijini, kata ya Maruku na Kanyangereko, vijiji vya Bulinda na Butayaibega. Kwa mujibu wa taarifa hizi, **jumla ya watu 7** wanasadikika walipata dalili za homa, kutapika, kutokwa damu maeneo mbalimbali ya mwili na figo kushindwa kufanya kazi. Aidha, **watu 5 kati yao wamefariki** na wengine **wawili 2 wako hospitali** wanaendelea na matibabu. Mwenendo wa ugonjwa huu unaashiria uwezekano kuwa ni ugonjwa wa kuambukiza.

Ndugu wananchi, Serikali inaendelea kufuatilia kwa karibu kuhusu mwenendo wa ugonjwa huu na kuchukua hatua za kudhibiti ili usisambae. Hatua hizi ni pamoja na;

- a) Sampuli kutoka kwa wagonjwa na waliofariki zimechukuliwa ili kubaini chanzo na kuthibitisha aina ya ugonjwa huo.
- b) Ufuatilaji wa watu wenye viashiria vya ugonjwa kwenye jamii na vituo vya kutolea huduma za afya pamoja na waliotangamana na wagonjwa hao ili kuwapa huduma stahiki za kimatibabu.
- c) Timu za kitaalamu za kukabiliana na mlipuko (Rapid Response Team) ngazi ya Mkoa na Halmashauri zimetumwa katika maeneo yaliyoathirika na zinaendelea na uchunguzi na hatua za udhibiti.
- d) Dawa, vifaa na vifaa tiba muhimu viro katika vituo vya kutolea huduma za afya mkoani Kagera na wagonjwa wanaendelea na matibabu.
- e) Elimu ya afya inaendelea kutolewa kwa jamii katika mkoa wa Kagera ili kuchukua tahadhari.

Ndugu Wananchi, Wakati Serikali inafuatilia mwenendo wa ugonjwa na kuchukua hatua za udhibiti, naomba muendelee kuwa watulivu na kuchukua hatua zifuatazo;

- a) Mtu ye yeyote mwenye dalili za homa, kutapika, kuharisha, kutoka damu na mwili kuishiwa nguvu anashauriwa kuwahi kituo cha kutolea huduma za afya mapema kwa ajili ya uchunguzi na matibabu.
- b) Kutoa taarifa mapema kwenye kituo cha kutolea huduma kilicho karibu au kupiga **simu namba 199** bila malipo endapo utamuona au kukutana na mtu mwenye dalili kama hizo.
- c) Kuepuka kumgusa mgonjwa au majimaji ya mwili mfano mate, machozi, damu, mkojo na kinyesi yatokayo kwa mgonjwa au mtu ye yeyote mwenye dalili hizo.
- d) Iwapo itakulazimu kumhudumia mgonjwa kwa dharura, chukua tahadhari ya kujikinga na majimaji yoyote kabla ya kumhudumia.
- e) Kunawa mikono mara kwa mara kwa maji tiririka na sabuni au kutumia vitakasa mikono ili kujikinga na magonjwa yote ya kuambukiza.
- f) Kuepuka kusalimiana kwa kushikana mikono.
- g) Kushirikisha wataalam wa afya katika shughuli za misiba na mazishi katika kipindi hiki.

Aidha, natumia nafasi hii kuwakumbusha watumishi wa afya kuzingatia kanuni za kujikinga na magonjwa ya kuambukiza (IPC) wakati wa kutoa huduma.

Ndugu wananchi, Serikali inatoa pole kwa familia zilizoondokewa na wapendwa wao. Aidha, nihitimishe kwa kuwaondoa hofu watu wote na kuwaomba kuwa watulivu wakati Wizara inaendelea kufuatilia kwa karibu na kuchukua hatua za udhibiti. Tutaendelea kuwapa taarifa za mwenendo wa ugonjwa huu.

Imetolewa na;

Prof Tumaini J. Nagu

MGANGA MKUU WA SERIKALI